TANGAZO LA SERIKALI NA. 260 la tarehe 24/7/2009

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

---

# SHERIA NDOGO

---

*Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 13(1)*

---

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO, 2009

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, 2009 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Jina na mwanzo wa kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililoko chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto. Eneo la Matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo- Tafsiri

"Afisa Muidhinishwa" maana yake ni Afisa ye yote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kutekeleza Sheria Ndogo hizi.

"Bidhaa" maana yake ni kitu cho chote kinachouzwa sokoni, mnadani au gulioni.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto.

"Mazao" maana yake ni mazao yoyote yanayotoka shambani au bustanini.

"Mifugo" maana yake ni pamoja na ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda na nguruwe.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto ikiwa ni pamoja na afisa ye yote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Mnada" maana yake sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuzia na kununulia mifugo.

"Mnunuzi" maana yake mtu, taasisi, kampuni au kikundi cho chote kinachojishughulisha na ununuzi wa mazao au mifugo.

"Muuzaji" maana yake mtu, taasisi, kampuni au kikundi cho chote kinachojishughulisha na uuzaji wa mazao au mifugo

"Soko" maana yake sehemu au eneo maalum lililotengwa kwa shughuli za kuuza na kununua bidhaa mbalimbali na ni pamoja na gulio.

"Madini" maana yake mchanga, kokoto, mawe, kifusi na chokaa.

"Kuchimba" ni pamoja na kukusanya.

"Ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri na mtu ye yote atakayeomba kukodi au kutumia mali ya Halmashauri.

"Mali ya Halmashauri" maana yake mali zote zilizo chini ya mamlaka ya Halmashauri na ni pamoja na vibanda, ukumbi, mitambo, majani na nyumba za makazi.

"Ushuru" ni pamoja na ushuru unaotozwa kwenye minada, soko, na ushuru wa mazao.

Ushuru

4.–(1) Halmashauri inaanzisha na kutoza ushuru wa masoko na minada utakaotozwa kwa muuzaji ye yote atakayeuza bidhaa zake kwenye masoko au minada hiyo kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la kwanza mpaka la tano la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu ye yote atakayelipa Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atawajibika kudai risiti kulingana na kiasi cha malipo yaliyofanyika.

(3) Ni marufuku kwa mtu ye yote kuuza au kununua bidhaa nje ya maeneo yaliyotengwa kama soko au gulio.

(4) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa chini ya kifungu cha (1) Halmashauri inaweza kuanzisha maeneo mengine kuwa masoko au minada kadri itakavyoona inafaa na masoko au minada hiyo itahesabiwa kama sehemu ya Sheria Ndogo hizi.

Msimamizi wa soko

5.–(1) Kutakuwa na Mkuu wa soko au mnada katika kila soko au mnada ambaye atakuwa ndiye msimamizi wa shughuli zote katika soko au mnada husika.

(2) Mkuu wa soko atakuwa na kazi zifuatazo:-

(i) msimamizi mkuu wa soko au mnada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kutoa maelekezo yanayotolewa na Halmashauri ikiwa ni pamoja na kutunza usafi wa soko ili kurahisisha ufanyikaji wa biashara kwenye soko au mnada;

(ii) kutoa amri ya kuondolewa mfugo ulioathirika na magonjwa,

(iii) kumtoa nje ya soko mtu ye yote atakayekataa au kushindwa kutekeleza maelekezo ya mkuu wa soko au mnada.

Ushuru wa taksi

6.–(1) Halmashauri itatoza ushuru kwa ajili ya taksi zinazofanya biashara ndani ya eneo la Halmashauri.

(2) Ushuru huo utakuwa shilingi 500/= kwa kila taksi kwa siku au shilingi 15,000/= kwa kila taksi kwa mwezi na utalipwa kila tarehe ya mwanzo wa mwezi na mlipaji atapatiwa stika maalum itakayobandikwa kwenye gari lake kuonyesha kuwa amelipa ushuru huo.

(3) magari yote yanayofanya kazi ya taksi lazima yasajiliwe na Halmashauri na kubandikwa namba ubavuni.

Ushuru wa stendi

7. Halmashauri itatoza ushuru kwa magari yote yanayoingia katika stendi kuu ya mabasi. Ushuru huo utakua shilingi elfu moja (1,000) kwa magari makubwa na shilingi mia tano (500/=) kwa magari madogo kwa siku.

Kodi ya vibanda

8.–(1) Halmashauri itatoza kodi katika kila kibanda kinachomilikiwa na Halmashauri pamoja na vibanda vyote vinavyozunguka soko la kibaya, uwanja wa mpira na stendi kuu ya mabasi kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la nne la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu ye yote atakayetaka kukodisha kibanda kinachomilikiwa na Halmashauri atalazimika kuingia mkataba na Halmashauri kwa makubaliano na masharti yatakayokuwepo kwenye mkataba huo.

(3) Muda wa mpangaji utakapoisha, mpangaji atalazimika kurudisha kibanda hicho kikiwa katika hali nzuri na kama bado anahitaji atalazimika kuingia mkataba upya na Halmashauri.

(4) Mwezi mmoja kabla ya muda wa mpangaji kumalizika Halmashauri ya wilaya itakagua vibanda vyake vyote kwa lengo la kufanya tathmini ya hali halisi ya vibanda hivyo.

(5) Endapo itagundulika kuwa kibanda cha mpangaji ye yote kimeharibika au hakiko kwenye hali nzuri na uharibifu huo umetokana na uzembe wa mpangaji, mpangaji huyo atalazimika kukikarabati kibanda hicho kwa gharama zake binafsi.

Uteuzi wa wakala

9.-(1) Halmashauri inaweza kumteua mtu binafsi, kampuni au Taasisi kuwa wakala wa kukusanya Ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha (1) atatakiwa kuwasilisha ushuru kwa Halmashauri kwa muda, kiasi na masharti watakayokubaliana katika mkataba.

Muda wa soko

10. Soko litakuwa wazi kuanzia saa kumi na mbili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili jioni katika siku zilizoainishwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Udhibiti wa magari

11.-(1) Ni marufuku kwa magari yote kuingia eneo la soko au mnada isipokuwa wakati wa kushusha na kupakia mizigo.

(2) Gari lenye mizigo litatakiwa kushusha mizigo na kuondoka eneo la mnada au soko baada ya kushusha na kupakia mizigo.

(3) Ni marufuku kwa mtu ye yote kupanda baiskeli ndani ya eneo la mnada au soko isipokuwa kwa walemavu wanaotumia baiskeli.

Vibanda

12.-(1) Kutakuwa na vibanda ambavyo vitatengwa maalum kwa ajili ya kuuzia nyama katika kila soko na mnada.

(2) Vibanda na sehemu za kuuzia nyama vitakuwa vinakaguliwa na Afisa Afya wa Halmashauri aliyeidhinishwa kufanya kazi hiyo kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Ada

13. Halmashauri itatoza ada kwa ajili ya kukodi au kutumia mali za Halmashauri kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la saba la Sheria Ndogo hizi.

Madini ya ujenzi

14. Ni marufuku kwa mtu ye yote kuchimba, kuanzisha mgodi, kumiliki au kukusanya madini ya ujenzi kama yalivyoorodheshwa kwenye jedwali la saba la Sheria Ndogo hizi bila kuwa na kibali kutoka Halmashauri.

Makosa na Adhabu

15. Mtu ye yote:-

(a) atakayekataa au kukwepa kulipa ada au ushuru,

(b) atakayemshawishi mtu au kundi la watu wasilipe ushuru au ushuru,

(c) atakayechimba madini ya ujenzi bila kibali,

(d) atauza bidhaa nje ya eneo lililotengwa kama soko au mnada.

Mtu ye yote atakayetenda kinyume na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atashitakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela (12) au adhabu zote mbili faini na kifungo na kulipa ushuru au ada yote anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

MINADA

| SAFU YA KWANZA | SAFU YA PILI | SAFU YA TATU |
|---|---|---|
| *Jina la Kata* | *Jina la Mnada* | *Tarehe kila Mwezi* |
| Dosidosi | Mnada wa dosidosi | 1 na 14 |
| Kibaya | Mnada wa kibaya | 2 na 15 |
| Ndedo | Mnada wa ndedo | 13 |
| Kijungu | Mnada wa kijungu | 3 na 16 |
| Lengatei | Mnada wa Lengatei | 4 na 18 |
| Sunya | Mnada wa Sunya | 6 na 20 |
| Dongo | Mnada wa kijiji cha laiseri | 5 na 19 |

JEDWALI LA KWANZA

| SAFU YA KWANZA | SAFU YA PILI |
|---|---|
| *Aina ya Mnyama* | *Kiwango (TSHS)* |
| 1. Ng'ombe | 5000 (kwa ng'ombe mmoja) |
| 2. Mbuzi | 2000 (kwa mbuzi mmoja) |
| 3. Kondoo | 2000 (kwa kondoo mmoja) |

JEDWALI LA TATU

MASOKO

| SAFU YA KWANZA | SAFU YA PILI |
|---|---|
| *Jina la kata* | *Tarehe (kwa wiki)* |
| 1. Matui | kila Ijumaa |
| 2. Njoro | kila Jumamosi |
| 3. Engusero | kila Jumatano |
| 4. Dongo | kila Jumamosi |
| 5. Songambele (Magungu) | kila Jumamosi |

JEDWALI LA NNE

MAZAO

| SAFU YA KWANZA | SAFU YA PILI |
|---|---|
| *Aina ya Mazao* | *Kiwango (Tshs)* |
| 1. Mahindi | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 2. Maharage | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 3. Alizeti | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 4. Mtama | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 5. Ngano | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 6. Ulezi | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 7. Choroko | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 8. Njegere | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 9. Ngwara | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 10. Kunde | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 11. Ndizi | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |
| 12. Mbaazi | Asilimia 5 ya bei ya mauzo |

Tangazo la Serikali Na. 260 (linaendelea)

JEDWALI LA TANO

BIDHAA ZINAZOUZWA SOKONI, MNADANI

| SAFU YA KWANZA | SAFU YA PILI |
|---|---|
| *Aina ya Bidhaa* | *Kiwango* (TSHS.) |
| 1. Vyakula /Chai | 200 (kwa siku) |
| 2. Vinywaji baridi/Bia | 500 (kwa siku) |
| 3. Mboga na matunda | 200 (kwa siku) kwa meza moja |
| 4. Pombe za kienyeji | 500 (kwa siku) |
| 5. Bdhaa za uhunzi (arts and crafts) | 200 (kwa siku) |
| 6. Kuchinja ng'ombe na kukagua | 4,500 (kwa kichwa) |
| 7. Kuchinja mbuzi na kondoo | 1000 (kwa kichwa) |
| 8. Mitumba | 500 kwa siku) |

JEDWALI LA SITA

MADINI

| *Aina ya Madini* |
|---|
| 1. Michanga |
| 2. Mawe |
| 3. Kokoto |
| 4. Kifusi/udongo |
| 5. Chokaa |
| 6. Changarawe (moramu) |
| 7. Udongo wa chumvi/mfinyazi) |

*Tangazo la Serikali Na. 260 (linaendelea)*

JEDWALI LA SABA

MALI ZA HALMASHAURI

| SAFU YA KWANZA | SAFU YA PILI |
|---|---|
| Aina ya Mali | Kiwango (TSHS.) |
| 1. Mashine ya hydro-form | 50,000 kwa siku |
| 2. Greda | 350,000 kwa siku |
| 3. Buldoza | 850,000 kwa siku |
| 4. Magari (a) madogo | 1,000 kwa kilomita moja |
| (b) makubwa | 1,000 kwa kilomita moja |
| 5. Vibanda vya Halmashauri | 10,000 kwa mwezi (kodi ya pango) |
| 6. Ukumbi wa Halmashauri | 70,000 kwa siku |

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya kiteto imewekwa kwa mujibu wa azimio la Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto katika kikao chake cha tarehe 29/01/2008 na nembo imewekwa mbele ya:-

FESTO L. KANG'OMBE,
*Mkurugenzi Mtendaji (w)*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto*

L.S.

MUSTAFA LESSY,
*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto*

NAKUBALI,

Dodoma
18 Mei, 2009

MHE.MIZENGO KAYANZA PETER PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto imewekwa kwa mujibu wa azimio la Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto katika kikao chake cha terehe 29/1/2008 na nembo imewekwa mbele ya:-

FESTO L. KANG'OMBE,
*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya Kiteto*

L.S.

MUSTAFA LESSY,
*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Kiteto*

NAKUBALI,

Dodoma
25 Julai, 2008

MHE. MIZENGO KAYANZA PETER PINDA,
*Waziri Mkuu*

---

TANGAZO LA SERIKALI NA. 239 la tarehe 24/10/2008

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290))

## SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1), 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (ADA ZA VIBAO VYA MATANGAZO YA BIASHARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO, 2008

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Halmashauri ya Kiteto za (Ushuru wa Vibao vya Matangazo ya Biashara) na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la serikali.

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya halmashauri ya Wilaya ya Kiteto.

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhinishaji" maana yake ni pamoja na Afisa Biashara wa Halmashauri ya au Wasaidizi wake, Mhandisi wa Ujenzi wa mji na Afisa mwingine yeyote atakayeteuliwa na Mkurugenzi kutekeleza Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto.

"Matangazo" maana yake ni maandishi yoyote yaliyoandikwa au kubandikwa kwenye vibao, ukuta wa jengo, au chombo chochote kwa ajili ya kutangaza biashara.

"Mfanyabiashara" maana yake ni mtu yeyote anayefanya biashara yoyote chini ya Sheria ya leseni za biashara au sheria yoyote andishi au sheria ndogo za Halmashauri.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa halmashauri ya Wilaya ya Kiteto na ni pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayekuwa ameteuliwa au kukasimiwa shughuli za Mkurugenzi.

"Vibao vya Matangazo" maana yake mbao, ukuta au mahali popote na chombo chochote ambacho kimewekwa tangazo la biashara.

4.-(1) Mfanyabiashara yeyote ambaye ameweka kibao cha matangazo ya biashara katika maeneo ya Halmashauri atatakiwa kulipia ada ya vibao vya matangazo.

5.-(1) Itakuwa halali kwa Afisa Mwidhiniwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mfanyabiahsara yeyote ambaye atashindwa kulipa ada ya vibao vya matangazo chini ya sheria ndogo hizi kumtaka alipe ada hiyo katika muda utakaooneshwa katika taarifa hiyo.

(2) Endapo mfanya biashara huyo atashindwa kulipa ada hiyo katika muda uliotajwa katika taarifa, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuondoa tangazo hilo na kudai gharama za kuondoa tangazo hilo kutoka kwa mfanyabiashara huyo na atakuwa na uwezo wa kumchukulia hatua za kisheria kwa kumfikisha mahakamani.

(3) Bila kuathiri masharti ya sheria ndogo hizi Halmashauri inaweza kudai ada za matangazo kwa njia ya kufungua kesi ya madai au jinai Mahakamani.

6.-(1) Itakuwa halali kwa afisa mwidhiniwa yeyote wakati wa kuingia katika eneo lolote wakati wa masaa ya kazi na kufanya ukaguzi kuona utekelezaji wa sheria ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote atakayemzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake atakuwa ametenda kasa.

7. Mtu yeyote ambaye atavunja sheria ndogo hizi au kushindwa kutekeleza maagizo yatakayotolewa chini ya sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

---

JEDWALI

---

USHURU WA MATANGAZO

(i) Vibao vilivyowekwa eneo la Mamlaka ya Halmashauri:

(a) Vibao vinavyong'aa Shs. 1,500 kwa kila mita ya mraba
(b) Vibao visivyong'aa Shs. 1,000 kwa kila mita ya mraba

(ii) Matangazo ya biashara kwa kutumia vipaza sauti Shs 20,000/= kwa siku

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto imewekwa kwa mujibu wa azimio la Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto katika kikao chake cha terehe 29/1/2008 na nembo imewekwa mbele ya:-

FESTO L. KANGOMBE,
*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya Kiteto*

L.S.

MUSTAFA LESSY,
*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Kiteto*

NAKUBALI,

Dodoma
25 Julai, 2008

MHE. MIZENGO KAYANZA PETER PINDA,
*Waziri Mkuu*

Tangazo la Serikali Na. 238 la tarehe 24/10/2008

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(Sura ya 288)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 153*

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO ZA MWAKA 2008

## SEHEMU YA KWANZA
### Utangulizi

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Jina

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto. Matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo; Tafsiri

"Afisa Mwidhinishwa" maana yake ni Afisa maliasili, Afisa kilimo na mifugo, Afisa Afya pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Eneo la Hifadhi: ni maeneo ya milima, mbuga za wanyama, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto;

"Hifadhi ya Mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na afisa mwidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yeyote;

"Kiwanda" maana yake ni jengo au kundi la majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa;

"Kuvuna misitu" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kung'oa miti na visiki;

"Maeneo ya malisho" maana yake ni pamoja na sehemu zote ambazo

zimetengwa na Halmashauri;

"Maji" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ni pamoja na maji ya kunywa, ya mito, vijito, maji yanayotiririka, yaliyohifadhiwa, yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maziwa, maji yaliyoko chini ya ardhi, na maji yaliyoko katika mkondo;

Maji taka" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. ....ya Mwaka 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na jasho, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi, majengo ya biashara na viwandani;

"Mazao ya misitu" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 chini ya kifungu Na. 2 ni kitu chochote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na miti, mazao yanayoota au kupatikana msituni, ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi, utomvu, maranda, matete, kamba, makuti (mawale), nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kusicho na uhai kitakachotangazwa katika gezeti la Serikali kuwa ni zao la msitu;

"Mazingira" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira 2004 yanahusisha maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe, hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za Kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana;

"Mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri;

"Mifugo" maana yake ni mifugo yoyote inayofugwa na binadamu;

"Misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi ya vichaka, na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

"Taka" Kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichojifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka;

"Taka Ngumu" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi mazingira ya Mwaka 2004 ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastic au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps).

"Taka za Viwandani" kama ilivyotafisiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, maana yake ni:-

Uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyinginezo ngumu kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004 sehemu ya IX.

"Uchafu Hatari" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani,au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia,kwa binadamu au mazingira.

"Uchafuzi wa Mazingira" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ni mabadiliko ya hali ya hewa ya moja kwa moja au yasiyo moja kwa moja, joto, kemikali, biolojia, au zana za mionzi katika mazingira ambayo zana hizo zinafanyia kazi au kutoa harufu mbaya, mrundikano wa taka ambao unaathiri watumiaji, au unaosababisha hali ya hatari kwa afya ya jamii, usalama, au ustawi, au hatari kwa wanyama, ndege, wanyama pori, samaki, au viumbe vyote vya baharini, mimea au kusababisha hali mbaya ya hewa, upungufu, au kizuizi ambacho ni sehemu katika sheria hizi.

"Udongo" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni pamoja na dunia, mchanga, miamba, miamba tope, madini, uoto wa mimea, mimea na wanyama iliyoko chini ya udongo pamoja na vumbi;

"Vitu hatari" maana yake kama ilivyotafasiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, ni kemikali yoyote, taka gesi, madawa, vidonge, mimea, wanyama au viumbe hai visivyoonekana ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA PILI
### MASHARTI YA UFUGAJI

Wajibu wa mfugaji

4. Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi:–

(a) atatakiwa kufuga idadi ya mifugo kama itakavyoamriwa na Halmashauri husika;

(b) ufugaji unaoruhusiwa kwa mijini ni ule wa ndani yaani (Zero grazing;

(c) atatakiwa kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri.;

(d) atatakiwa kupitisha mifugo yake katika njia (stock routes) zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;

(e) atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;.

(f) atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na halmashauri;

(g) atatakiwa kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;

(h) atatakiwa kuchangia gharama za ukarabati wa majosho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;

(i) atatakiwa kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;

(j) atatakiwa kuweka alama kwenye mifugo yake (Branding, ear tags) na katika viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi;

(k) atatakiwa kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyo hitajiwa na Halmashauri;

(l) kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbung'o.

Masharti kwa mfugaji

5. Ni marufuku kwa mfugaji yeyote:

(a) kuchunga, kulisha,au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hiyo;

(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;

(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri;

(d) kibali cha kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri kitatolewa na afisa kilimo na mifugo;

(e) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri;

(f) kufuga mifugo mingi katika eneo dogo la Halmashauri;

(g) ni marufuku kwa mfugaji yeyote kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri kupitisha mifugo.

Kud- mifu- inaye- ovy-

6.-(1) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashauri ya Mji ambapo hapajaruhusiwa kuchungia mifugo.

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa utalipiwa faini na gharama nyingine zitakazojitokeza kama itakavyoamriwa na Halmashauri, baada ya kulipia hizo gharama atarudishiwa mifugo yake.

(3) Endapo mwenye mifugo au mfugo hatatokea ndani ya kipindi kilichowekwa na Halmashauri tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo na kama hataonekana ndani ya muda uliopangwa na halmashauri fedha hizo zitaingizwa katika vyanzo vya mapato ya Halmashauri.

(5) Endapo mwenye mifugo hiyo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake katika muda uliopangwa na Halmashauri, halmashauri itarudhisha fedha zake.

(6) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo au mfugo Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote.

Ukaguzi wa mifu-

7.-(1) Itakuwa halali kwa afisa kilimo na mifugo, maafisa watendaji wa kata na vijiji/mitaa, na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kuingia katika nyumba au

jengo lolote wakati wowote kwa madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya mifugo iliyomo katika nyumba hiyo.

(2) Mtu yeyote atakaye wazuia maafisa waidhinishwa katika kifungu cha 7(1) kutekeleza wajibu wao chini ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa Halmashauri

8.–(1) Ni wajibu wa kila Halmashauri kutenga maeneo maalumu Kwa ajili ya shughuli za kulisha na malisho na kwa kuzingatia idadi ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na 114 pamoja na Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na.20 ya Mwaka 2004.

(2) Halmashauri itatenga njia maalumu ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni, Minadani.

(3) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Taratibu za ufugaji

9.–(1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika Sheria Ndogo hizi au Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo/mnyama wake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana. Hairuhusiwi mtu yeyote kuchinjia nyama na mfugo mahali pengine popote.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yeyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri ya mji isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo na Halmashauri.

## SEHEMU YA TATU
### KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI

Taratibu za kilimo

10.–(1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia sheria ya Ardhi sura ya 113 na 114 na Sheria nyingine zitakazotungwa na Bunge.

(2) Itakuwa halali kwa Halmashauri kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo itakayotungwa na Halmashauri.

(3) Haitaruhusiwa kulima mazao marefu katika maeneo ya mijini.

Masharti kwa mkulima

11.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima katika Miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakalo haribu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia ushauri wa Afisa wa Kilimo.

(2) Ni marufuku kwa mitu yeyote kutumia kinyume ardhi iliyotengwa kwa matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka kwa Halmashauri.

(4) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(5) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4.00 usiku.

(6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za Kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia Kilimo cha kuhamahama na kuhimiza Kilimo cha mzunguko (crops rotation).

Uhifadhi wa Uoto wa asili

12. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.

Uchimbaji mchanga na kokoto

13.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kando kando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa ruhusa maalumu ya Halmashauri.

14. Ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo la hifadhi.

## SEHEMU YA NNE
### HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa Halmashauri Kulinda vyanzo vya maji

15.-(1) Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yoyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

Kulinda eneo la hifadhi

16.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha Maji isipokuwa Halmashauri husika tu.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

17.-(1) Ni marufuku kwa mtu yoyote, Kiwanda, Taasisi, Shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, visima, mifereji, chemichemi au sehemu yoyote ambayo ni Chanzo cha Maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.

## SEHEMU YA TANO
### HIFADH YA MISITU

Kuchoma au kusababisha moto

18.-(1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuchoma moto misitu kwa namna yoyote ile katika Misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, Kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka

kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

19. Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto atalazimika kutoa taarifa kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma moto kabla ya siku saba (7) na ataweka njia za kuzuia moto. Kibali c kuchom moto

20.-(1) Hairuhusiwi kwa mtu yeyote kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri. Ukataji miti

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali kwa Taifa.

(4) Watu wanao vuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri husika kwa ajili ya kuchoma mkaa.

21. Kila Mkazi wa Halmashauri atawajibika kupanda na kutunza miti katika eneo lake kama atakavyoelekezwa na Halmashauri. Wajibu w kupanda miti

(a) kupanda na kutunza miti katika makazi yake kama atakavyoelekezwa na Halmashauri;
(b) kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki.

22. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi: Wajibu wa kutenga Eneo la hifadhi ya misitu

(a) kila kijiji kitawajibika kutenga eneo la hifadhi ya Msitu wa asili (Ndobido) kwa ajili ya matumizi ya baadaye.
(b) kila kijiji kitalazimika kutunza miti yote inayopandwa katika eneo la Kijiji.
(c) kila kijiji kitahakikisha ya kuwa kila kaya inapanda miti

isiyopungua kumi kwenye eneo la nyumba yake.

(d) mtu yeyote anayetaka kukata miti/mti wa matumizi ya kuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi na shughuli nyingenezo, itabidi kupata kibali cha maandishi toka kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kijiji na kibali cha Afisa Maliasili wa Halmashauri au Wasaidizi wake kwa miti iliyopandwa na kuhifadhiwa na Halmashauri ya Wilaya.

(e) kila kijiji kitapaswa kutenga na kupanda shamba la miti ekari 2 kila mwaka na kulitunza.

(f) kila Shule au Taasisi nyinginevyo katika halmashauri ya Wilaya itapaswa kupanda miti ya kukinga upepo kuzunguka majengo yake na kuwa na shamba lisilopungua miti hekta 2.

(g) kijiji kitapaswa kutunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na vyanzo vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo.

(h) kijiji kitahakikisha kuwa kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake kama kinga upepo.

(i) kila mtu mwenye nyumba kwenye Halmashauri atawajibika kupanda miti kando ya barabara inayopita mbele ya nyumba yake na kuitunza.

(j) kila Mwenyekiti wa Kitongoji, mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kijiji, Mkuu wa Taasisi yoyote katika halmashauri ya Wilaya atahakikisha kuwa Kijiji, , Taasisi ina msitu wa hifadhi wa miti ya kupandwa au ya asili iliyotengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi ardhi, mazingia na matumizi ya baadaye.

## SEHEMU YA SITA
### TAKA NGUMU NA LAINI

23 (1) Ni wajibu wa kila Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake.

(2) Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini, au kujisaidia katika kingo, mito, mabwawa au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika halmashauri ya Wilaya ya Kiteto atakuwa ametenda kosa.

(3) Kila mwananchi au mkazi yeyote wa Kiteto ana wajibu wa kumkamata mwananchi yeyote au shirika lolote au kikundi cha watu

wowote watakaofanya shughuli zinazochafua mazingira, au kutupa taka ovyo, au kujisaidia mahali pasiporuhusiwa na kufikishwa kwa Mtendaji wa Kata na kulipishwa faini au kupewa adhabu kwa mujibu wa sheria Ndogo hii.

24. Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kuanika mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengi katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi. Uendeshaji wa viwanda

SEHEMU YA SABA

MAKOSA NA ADHABU

25.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa; Makosa na adhabu yanayohusu mifugo

(a) Ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali.
(b) Atasafirisha mifugo bila kuwa na kibali
(c) Atalisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa au
(d) Atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa,

√ 26. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, kokoto, madini katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa. Makosa yanayohusu kilimo

√ 27 Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kuhifadhi Ardhi atakuwa ametenda kosa. Makosa na adhabu yanayohusu kuhifadhi ardhi

√ 28.-(1) Mtu yeyote atakayeharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji atakuwa ametenda kosa. Makosa na adhabu yanayohusu vyanzo vya maji

(2) Mtu yeyote atakayebainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine ambao ni rasilimali ya Taifa atakuwa ametenda kosa.

29.-(1) Mtu yoyote atakuwa ametenda kosa ikiwa: Makosa yanayohusu uharibifu misitu

(a) atachoma au kusababisha moto katika misitu bila kibali;

(b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto au;
(c) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa, bila kibali au;:
(d) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali au;
(e) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;
(f) atachoma au kusababisha moto katika misitu bila kibali au.
(g) atashindwa kushiriki katika kuzima moto au;.
(h) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa/ isiyohifadhi, bila kibali au;
(i) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali au;
(j) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;
(k) kuchungia mifugo kwenye eneo lake lolote lililopandwa miti au iliyohifadhiwa kama bustani ya miti;
(l) kukata miti au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo;
(m) kubandua magome ya miti kwa ajili kutengeneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na kibali;
(n) kulima au kukata miti katika vyanzo vya maji, [illegible], kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

**Makosa yanayohusu taka ngumu na laini**

30. Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa na Sheria hii au Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atakuwa ametenda kosa.

**Makosa yanayohusu taka za majimaji**

31. Mtu yeyote atakayetiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai atakuwa ametenda kosa.

**Makosa yanayohusu viwanda**

32. Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji atakuwa ametenda kosa.

**Adhabu**

33. Mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atahukumiwa kulipa faini isiyozidi shilingi Laki tatu (Tshs.300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto imewekwa kwa mujibu wa azimio la Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto katika kikao chake cha tarehe 29/1/2008 na nembo imewekwa mbele ya:-

FESTO L. KANG'OMBE,
*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya Kiteto*

L.S.

MUSTAFA LESSY,
*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Kiteto*

NAKUBALI,

Dodoma
25 Julai, 2008

MHE. MIZENGO KAYANZA PETER PINDA,
*Waziri Mkuu*

---

TANGAZO LA SERIKALI NA. 239 la tarehe 24/10/2008

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290))

## SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1), 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (ADA ZA VIBAO VYA MATANGAZO YA BIASHARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO, 2008

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Halmashauri ya Kiteto za (Ushuru wa Vibao vya Matangazo ya Biashara) na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la serikali.